



10B-Kuleta Basmalah Wakati Wa Kuunga Bainaa Ya Suwrah Mbili:


1- **وصل الجميع Waswlul-jamiy' -Kuunganisha zote**: Kuiunganisha Aayah ya mwisho wa Suwrah ya kwanza na Basmalah na Aayah ya mwanzo wa Suwrah nyengine kwa kuzisoma zote mfululizo bila kusimama kama ifuatavyo:



2- **قطع الجميع Qatw'ul-jamiy' -Kutenganisha zote**: Kuzitenganisha Aayah ya mwisho wa Suwrah ya kwanza na Basmalah na Aayah ya mwanzo wa Suwrah nyengine; kwa kuzisoma moja baada ya nyengine kwa kusimama kila baada ya moja; kama ifuatavyo:



3- **وصل البسمة بالسورة Waswlul-basmalah bis-suwrah: Kuunganisha Basmalah na Suwrah ya mwisho**: Kuitenganisha kwa kuisoma Aayah ya mwisho wa Suwrah ya kwanza pekee kwa kusimama, kisha kuziunganisha Basmalah pamoja na Aayah ya mwanzo wa Suwrah nyengine.; kama ifuatavyo:



4- HAIPASI kuunganisha Aayah ya mwisho wa Suwrah ya kwanza na Basmalah ya Suwrah ya pili kwa kuzisoma kwa pamoja kisha ukasimama na ukaanza upya kuisoma Aayah ya kwanza ya Suwrah mpya. Hii ni kwa sababu inampelekea msikilizaji kudhania kwamba Basmalah ndio Aayah iliyomalizikia Suwrah iliyomalizwa kusomwa; na hali ya kuwa Basmalah haikuwekwa isipokuwa kusomwa mwanzo wa Suwrah. Kwa hivyo kusoma kama ifuatavyo ni makosa.



﴿ وَلَمْ يَكُنْ لَّهُ كُفُوًا أَحَدٌ ﴾ ﴿ قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ الْفَلَقِ ﴾ ﴿ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ﴾